Opportunities for Youth Employment

Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

Embassy of Switzerland in Tanzania
Ubalozi wa Uswisi Tanzania

# UBALOZI WA USWISI NA SNV KUTANUA MRADI WA AJIRA KWA VIJANA TANZANIA

***Dodoma, Juni 6, 2016*** **– Ubalozi wa Uswisi na SNV Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV) leo wametangaza ushirikiano katika kutanua mradi wa ajira kwa vijana Tanzania, "Opportunities for Youth Employment" (OYE) nchini Tanzania katika hoteli ya St. Gaspar mjini Dodoma. Mradi wa OYE unahusisha moja kwa moja serikali, sekta binafsi, asasi za kiraia na taasisi za kifedha kuhakikisha vijana wana ujuzi unaohitajika na waajiri, na kuwaunganisha na fursa mbalimbali za ajira au kujiajiri.**

Balozi wa Uswisi nchini Tanzania, Mheshimiwa Florence Tinguely Mattli, ameusifiwa mradi wa OYE kama mradi bunifu na wakipekee na ni njia nzuri ya kukuza ajira kwa vijana. "Uswisi imedhamiria kushirikiana na Tanzania katika kuimarisha mafunzo ya ufundi stadi ikiwa kama ni hatua ya kwanza katika utekelezaji wa dira yake kuunga mkono ajira kwa vijana na maendeleo ya biashara," alisema. "Kukuza fursa za ajira kwa vijana pamoja na ujasiriamali katika maeneo mbalimbali vijijini ni njia ya kuimarisha ukuaji wa uchumi Tanzania."

"Ajira kwa vijana ni miongoni mwa vipaumbele vya ofisi yangu," alisema Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mheshimiwa Jordan Rugimbana. "Napongeza juhudi wanazofanya washirika wetu wa maendeleo ili kuziba pengo la ukosefu wa ajira."

Mradi wa OYE ulizinduliwa na SNV na The MasterCard Foundation mwaka 2013 kwa lengo la kuboresha maisha ya vijana 20,500 ili kujenga fursa za ajira katika sekta ya kilimo na nishati mbadala nchini Tanzania, Rwanda na Msumbiji. Mpaka kufikia mwishoni mwa Machi mwaka huu, jumla ya vijana 13,407 - asilimia 40 wakiwa ni wasichana - wamejiunga na mradi wa OYE, na 12,403 wamekamilisha mafunzo ya stadi za maisha na kiufundi, na biashara. Asilimia 72 (8,945) ya waliomaliza mafunzo haya wana ajira endelevu au wameanzisha biashara zao wenyewe.

"Vijana wengi wanajishughulisha na kazi na biashara za aina tofauti na mara nyingi hawategemei kazi au biashara moja tu," alisema Roy van der Drift, Meneja wa Programu ya OYE katika la Shirika la Maendeleo la Uholanzi SNV. "Tunafanya kazi ili kuhakikisha changamoto hii ya ajira inatatuliwa kwa kutoa ujuzi unaohitajika na vijana ili kuwapa ajira waweze kujikimu kimaisha."

Kwa mujibu wa Benki ya dunia, takribani asilimia 32 ya watu Tanzania ni vijana wenye umri kati ya miaka 15 na 34, na inakadiriwa kuwa takribani asilimia 13.4 ya nguvu kazi ya vijana wote hawana ajira. Hata hivyo, tatizo kubwa zaidi ni 'kufanya kazi kwenye mazingira magumu' kwa wafanyakazi wa majumbani na waliojiajiri. Nchini Tanzania, 'wanaofanya kazi kwenye mazingira magumu' wanakadiriwa kuwa ni asilimia 88.

"Hii ni fursa ya kipekee ya kutanua mradi wa OYE na faida zake" alisema Alemayehu Konde Koira, Meneja mwandamizi wa programu ya maisha ya vijana katika shirika la The MasterCard Foundation. "Tunafurahishwa na uongezekaji wa ushirikiano baina ya washirika wa maendeleo kwenye njia bunifu za ajira kwa vijana ambazo zitanufaisha maelfu ya vijana walioko vijijini nchini Tanzania.

Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi litachangia zaidi ya dola za kimarekani milioni nne nukta saba (4.7) ili kukuza na kuendeleza mradi kwa mikoa mitano ya Dodoma, Manyara, Singida, Tabora na Shinyanga vijijini Tanzania na kuongeza idadi ya vijana amabo hawako shuleni elfu 5 mia tano (6,500) watakaowezeshwa kiuchumi.

###

**Kuhusu SNV Shirika la Maendeleo la Uholanzi**
SNV ni shirika la kimataifa la maendeleo lisilo la kibiashara lenye rekodi ya muda mrefu katika nchi 38. SNV inaamini kwamba hakuna mtu anapaswa kuishi katika umasikini na kwamba watu wote wanapaswa kuwa na nafasi ya kuweza kujiendeleza. Kwa maelezo zaidi tembelea: http://www.snv.org/

**Kuhusu Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi**
Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi (SDC) lina wajibu wa urabitu wa jumla wa shughuli za maendeleo pamoja na misaada ya kibinadamu inayotolewa na nchi ya Uswisi. Nchini Tanzania, Uswisi inachangia mapambano dhidi ya umasikini katika ukanda wa kati. Wakati Uswisi husaidia kuwezesha upatikanaji wa huduma bora za afya, pia inasaidia kukuza kipato na kujenga fursa za ajira katika maeneo ya vijijini pamoja na kuimarisha asasi za kiraria na vyombo huru vya habari . Kwa habari zaidi , tafadhali tembelea: https://www.eda.admin.ch/daressalaam

**Kuhusu The MasterCard Foundation**
The MasterCard Foundation The MasterCard Foundation inashirikiana na mashirika yenye dira kwenye utoaji na uwezeshaji wa elimu, mafunzo ya stadi na huduma za kifedha zikilenga jamii masikini hasa katika ukanda wa Afrika. Likiwa ni miongoni mwa mashirika makubwa yanayojitegemea, kazi zake zinaongozwa na dhima ya kuboresha mafunzo na kuwezesha jamii kifedha ili kupunguza au kuondokana na umasikini. Makao makuu ya shirika yakiwa Toronto, Canada. Shirika hili lilianzishwa rasmi na MCF mnamo mwaka 2006. Kwa maelezo Zaidi jiunge na jarida letu, Pia tembelea tovuti yetu www.mastercardfdn.org. Tufuate kwenye mtandao wetu wa kijamii wa twitter @MCFoundation.

***Kwa mawaliniano:***

*Corjan van der Jagt, OYE Tanzania Project Manager, SNV Netherlands Development Organisation*
*Tel: +255 22 260 0340; Email: cvanderjagt@snvworld.org*

*Roy van der Drift, OYE Program Manager (Tanzania, Mozambique, Rwanda), SNV Netherlands Development Organisation*
*Tel: +255 688009351; Email: rvanderdrift@snvworld.org*

*Sheila Ally, Communication Officer, Embassy of Switzerland in Tanzania*
*Tel: +255 22 266 6220, Email: sheila-suleiman.ally@eda.admin.ch*

*Kristy Tomkinson, Communications Associate, The MasterCard Foundation*
*Tel: +1 416-214-1426; Email: ktomkinson@mastercardfdn.org*